JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

# KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM

## SHAURI LA UKIUKAJI WA AGIZO LA SERIKALI KUHUSU KUTOSOMA HABARI ZA MAGAZETINI KWA UNDANI

## SHAURI NA. 06-2018/2019

## RADIO FREE AFRICA

# UAMUZI

## UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA AGIZO LA SERIKALI LA KUTOSOMA HABARI ZA MAGAZETINI KWA UNDANI

### 1.0 Utangulizi

1.1 Kituo cha Utangazaji cha Radio Free Africa cha Mwanza kinatuhumiwa kukiuka Agizo la Serikali lililotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (MB), tarehe 03 Mei, 2017 kwa watangazaji wa vituo vya Redio na Televisheni kutosoma kwa undani maudhui yaliyomo katika magazeti badala yake wasome vichwa vya habari pekee. Kimsingi, agizo hilo la serikali lililenga kulinda soko la biashara ya uchapishaji, usambazaji, na uuzaji wa magazeti nchini.

1.2 Aidha, tarehe 15 Juni, 2017, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) iliviandikia barua vituo vyote vya utangazaji (ikiwa ni pamoja na kituo cha Radio Free Africa) na kuvitaka kuacha mara moja kusoma kwa undani habari za magazetini na badala yake wasome tu vichwa vya habari kwa mujibu wa agizo hilo la serikali.

1.3 Tarehe 01 Februari, 2019, Kituo cha Radio Free Africa kilituhumiwa kukiuka kwa makusudi agizo hilo la serikali kupitia kipindi chake cha **"Good Morning Africa"** kwenye kipengele cha **"Tuzungumze Magazetini"** kilichorushwa kati ya saa 12.00 asubuhi na saa 03.00 asubuhi. Katika kipindi hicho, mtangazaji wa kipindi, Bwana Michael Noel alisoma kwa undani habari mbali mbali zilizoandikwa katika magazeti ya Habari Leo, Mwananchi, Nipashe, na Mtanzania kinyume na agizo lililotolewa na serikali.

1.4 Kitendo cha kusoma taarifa hizo za magazeti kwa undani ni kupuuza kwa makusudi agizo la Serikali lililotolewa na Mheshimiwa Waziri tarehe 03 Mei, 2017 jijini Mwanza

wakati wa kilele cha maadhimisho ya 26 ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari duniani.

1.5 Tarehe 05 Februari, 2019, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilikiagiza Kituo cha Radio Free Africa kuwasilisha CD ya Maudhui ya kipindi kilichotuhumiwa kukiuka agizo hilo la Serikali ili kisikilizwe na Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na kujiridhisha kama maudhui ya kipindi hicho na uwasilishaji wake ulikiuka agizo la Serikali au la.

1.6 Mtangazaji wa kipindi cha Good Morning Africa alikiuka Agizo hilo la Serikali kwa kusoma habari za magazetini kwa undani kama ifuatavyo:-

**Gazeti la Habari Leo**: *"Ndugai amlipua Lissu ambana Zitto... Spika wa Bunge Job Ndugai amevunja ukimya na kujibu tuhuma za upotevu wa shilingi trilioni 1.5 ambazo mbunge wa Kigoma Mjini Zitto Kabwe (ACT Wazalendo) alidai kuwa Mkaguzi na mdhibiti wa hesabu za serikali (CAG) amesema hazionekani matumizi yake na kudai kuwa mbunge huyo ni muongo. Katika hatua nyingine Bunge limebainisha kumlipa mbunge wa Singida Mashariki Tundu Lissu kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA takribani Shilingi milioni 250 kama malipo mbali mbali kwa kipindi cha mwaka mmoja na miezi mitatu ama kwa ujumla ni miezi 15. akimzungumza Zitto Bungeni jana mara baada ya kukamilika kwa kipindi cha maswali na majibu, Spika Ndugai alimsihi Zitto kuwa na hofu ya Mungu kwa kuacha kusema uongo kwa kuwa haipendezi mtu mzima kusema uongo kwa taifa na kimataifa."*

*"Biteko aibua madudu zaidi madini... Waziri wa madini Dotto Biteko amebaini madudu yanayofanywa na maofisa wake mjini Dodoma jambo ambalo lililomfanya Katibu mkuu kumsimamisha kazi papo hapo Ofisa Madini Hashim Daniel ili kupisha uchunguzi. Moja ya madudu yanayofanywa na wafanyakazi wa ofisi ya madini mkoa wa Dodoma ni kutokujaza uzito wa madini ama dhahabu unaopatikana baada ya uchenjuaji na badala yake kuruhusu uuzaji wa madini hayo kwa watu wasio na vibali jambo linalosababisha upotevu wa mapato ya serikali. Biteko alibaini hayo juzi jioni alipofanya ukaguzi wa kushtukiza katika moja ya vituo vya uchenjuaji wa madini eneo la Kizota jijini Dodoma".*

*"Mtoto afa kwa kuangukia chungu cha maharage... ni mwanafunzi aliyekuwa akisoma katika shule ya msingi Sintali Kata ya Sintali wilayani Nkasi mkoani Rukwa, Exavery Mwananjelwa mwenye umri wa miaka 5 amekufa baada ya kuanguka na kichwa chake kuzama kwenye chungu cha maharage yaliyokuwa yakichemka jikoni... "Akina mama muwe na tahadhari mnapokuwa kwenye mapishi angalieni watoto hawa wacheze mbali zaidi maana limekuwa tatizo tunajuzwa hapo mtoto afa kwa kuangukia chungu cha maharage yaliyokuwa yanachemka jikoni tuchukue tahadhari hasa tunapokuwa jikoni na watoto hawa".*

**Gazeti la Mwananchi**: *"Chadema, CCM na vita mpya ya kura milioni 4 ni kwa namna gani hapo unaweza kujipatia nakala yako ya gazeti hili kujua nini ambacho mwananchi imekibaini kuelekea uchaguzi mkuu mwaka 2020, Lakini nikudokeze tu hapo kwamba Chadema na CCM wamesema wanajipanga kuvuna wapiga kura wapya milioni 4 baada ya jana serikali kueleza bungeni kuwa kabla ya Uchaguzi Mkuu 2020 idadi hiyo ya wananchi wataandikishwa katika daftari la kudumu la wapiga kura, Chadema, CCM na vita mpya ya kura milioni 4 wapiga kura wapya hao kuelekea uchaguzi wa 2020".*

*"Hivi ndivyo Ma RC, DC walivyosweka watu ndani, mwananchi limedokeza hapa kuwa baadhi ya wakuu wa mikoa na wilaya wamekuwa wakiwasweka watu ndani katika matukio tofauti jambo ambalo limekuwa likipigiwa kelele na viongozi mbali mbali, ile unawekwa ndani saa 48 tumekuwa tukishuhudia pia matukio haya yakitokea kwamba Wakuu wa Wilaya na Mikoa kusweka watu ndani Mwananchi limedokeza hapa katika ukurasa wake wa mbele Hivi ndivyo MaRC, DC walivyosweka watu ndani."*

*"Sakata la matibabu ya Lissu laibuka upya...tunaambiwa kutoka jijini Dodoma na Dar es Salaam unaweza kusema sakata la matibabu ya Mbunge wa Singida Mashariki Tundu Lissu, limeibuka upya baada ya jana Spika Job Ndugai kusema bunge limemlipa stahili zake zinazofikia sh. milioni 250 huku mbunge huyo akisema mhimili huo wa dola haujawahi kutoa hata senti moja ya kugharamia matibabu yake...Ndugai ametoa kauli hiyo katika kipindi ambacho Lissu anaendelea na matibabu nchini Ubeligiji baada ya kushambuliwa kwa risasi Septemba 7, 2017 nje ya makazi yake area D jijini Dodoma. Tangu wakati huo mbunge huyu, familia yake pamoja na chama chake Chadema wamekuwa wakiulalamikia uongozi wa bunge kutogharamia matibabu yake lakini jana baada ya kipindi cha maswali na majibu bungeni Spika Ndugai alisema hadi mwishoni mwa Desemba mwaka jana Lissu alikuwa amelipwa sh. milioni 207.8 pamoja na sh. milioni 43 zilizotolewa kama mchango wa matibabu ya mbunge huyo."*

**Gazeti la Nipashe:** *"Zitto matatani kisa trilioni moja ni habari nyingine ambayo imedokezwa hapa kwenye ukurasa wa mbele wa gazeti la Nipashe kuhusiana na habari hii nikudokeze hapo ambayo imedokezwa kwenye gazeti hili la Nipashe Mwanga wa Jamii tunaambiwa kwamba, Spika wa Bunge Job Ndugai, amesema anamuweka kiporo Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto kabwe, kutokana na mbunge huyo wa Kigoma Mjini kwa tiketi ya ACT Wazalendo kuishikia bango kashfa ya madai ya ubadhilifu wa Sh. tirioni 1.5 zinazotajwa kwenye ripoti iliyopita ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)".*

*"Kiongozi huyo wa bunge amedai Zitto ni muongo lakini wakati wa kumpeleka mbele ya kamati ya maadili na madaraka ya bunge haujafika. Muda mfupi baada ya kipindi cha maswali na majibu bungeni Spika Ndugai akiwa anaongoza kikao hicho cha tatu cha mkutano wa 14 ... alimshukia Zitto kwa kitendo chake alichodai ni kuandika uongo katika ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram..."Huyu Zitto aliandika katika ukurasa wake wa Instagram kwamba CAG alikuwa amefanya ukaguzi hazina na katika ukaguzi huo wizi mkubwa wa ubadhilifu wa fedha wa sh. tirioni 1.5 na ametoa ripoti maalumu ya ukaguzi huo na ripoti hiyo imefika ofisi ya Spika na Spika amekalia ripoti hiyo," alisema. Ni nukuu hiyo ambayo imetoka bungeni mjini Dodoma".*

*"Nyoka wa ajabu aua watano Sumbawanga: eeee! mbona maajabu hayo kutoka huko Sumbawanga lakini ni habari ya kuhuzunisha kweli kweli maofisa maliasili wa Halmashauri ya wilaya Sumbawanga mkoani Rukwa wameamua kushirikiana na mtaalamu wa tiba za jadi wa kijiji cha Nambo Tarafa ya Milepa kumsaka nyoka wa ajabu anayedaiwa kuua kwa nyakati tofauti tofauti kijijini hapo". Diwani wa Kata ya Milepa Apolinary Macheta alisema jana nyoka huyo aina ya koboko kagonga na kusababisha vifo vya watu watano katika kipindi cha miaka minne tofauti... Ni habari ya kuhuzunisha kweli kweli lakini unaweza ukastaajabu aina ya nyoka huyo ambaye amesababisha vifo vya watu watano huko Sumbawanga ni gazeti la Nipashe ambalo limetudokeza".*

*"Masharti magumu kuzipata dola na Euro: Benki Kuu ya Tanzania BOT imesema kuanzia sasa huduma za kubadilisha fedha za kigeni zitapatikana katika mabenki na taasisi za kifedha zinazoendesha biashara nchi nzima. Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa jana kwa vyombo vya habari na BOT, benki na taasisi za fedha zinatakiwa kutoa huduma hiyo kwa wateja wote, benki kuu imehimiza benki na taasisi za fedha kuendelea kutoa huduma za kubadilisha fedha za kigeni kwa wateja wote wakati uchunguzi wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni na maduka bubu unaendelea. Ilisema taarifa hiyo".*

*"Kesi ya kina Mbowe yapata hakimu mpya... Ni kesi inayomkabili mwenyekiti wa taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Freeman Mbowe... tunaambiwa imepata jaji mpya, tunaambiwa kesi inayomkabili mwenyekiti wa CHADEMA Taifa Freeman Mbowe na wenzake nane wanaokabiliwa na mashitaka ya uchochezi imepata hakimu mpya...Jana kesi hiyo ya jinai namba 112/2018 ilitajwa mbele ya hakimu mkazi mwandamizi mfawidhi Kelvin Mhina katika mahakama ya hakimu mkazi kisutu jijini Dar es salaam awali kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa mbele ya hakimu mkazi mkuu wa mahakama hiyo Wilbard Mashauri ambaye sasa amepanda cheo na kuwa jaji wa mahakama kuu ya Tanzania".*

**Gazeti la Mtanzania:***"Mwanafunzi aliyepotea akutwa chini ya uvungu wa kitanda adai alikua anajiona anaenda shule walimu, polisi wazungumza...ni mwanafunzi wa kike wa kidato cha nne wa shule ya Sekondari Ikinabushu wilayani Bariadi jina linahifadhiwa na gazeti hili la Mtanzania... amekutwa chini ya uvungu wa kitanda nyumbani kwa bibi yake. Mwanafunzi huyo alikutwa kwenye eneo hilo akiwa hajitambui baada ya kupotea kwa siku tano tangu Januari 25, 2019 mpaka siku ya jana.... ni mwanafunzi aliepotea akutwa chini ya uvungu wa kitanda ni habari nyingine ambayo imedokezwa katika ukurasa wa mbele wa gazeti la Mtanzania fikra yakinifu."*

## 2.0 Wito wa kufika mbele ya Kamati ya Maudhui

Baada ya kuona ukiukwaji wa agizo hilo, tarehe 04 Aprili, 2019 Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa Radio Free Africa wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi kwa nini wasichukuliwe hatua. Wito pia uliutaka uongozi huo ulete utetezi wa kimaandishi.

Tarehe 11 Aprili, 2019, saa 06:00 mchana, uongozi wa Kituo cha Radio Free Africa uliitwa mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao kwa nini kituo hicho kisichukuliwe hatua kutokana na tuhuma za kukiuka Agizo la Serikali linalowataka watangazaji wa vituo vya Redio na Televisheni kutosoma kwa undani maudhui yaliyopo katika magazeti na badala yake wasome vichwa vya habari pekee. Katika kutoa utetezi wake, Radio Free Africa iliwakilishwa na Steve Diallo, Meneja Uendeshaji na Ufundi na Michael Noel, Mtangazaji.

## 3.0 Kusikiliza Kipindi cha Good Morning Africa

Kamati ya Maudhui na Uongozi wa Radio Free Africa walisikiliza kipindi cha Good Morning Africa cha tarehe 01 Februari, 2019 kilichorushwa na Radio Free Africa ili kujiridhisha iwapo kituo hicho kilikiuka agizo tajwa la serikali au la.

## 4.0 Maelezo ya Utetezi ya Radio Free Africa

Uongozi wa Radio Free Africa uliwasilisha utetezi wao wa maandishi kwa Kamati. Katika utetezi wao huo, Radio Free Africa wamekiri kosa na kuomba radhi wakisema

kuwa mtangazaji alitenda kosa hilo kutokana na kutokuwa na uzoefu na kipindi cha magazeti alichopangiwa kukitangaza kwa dharura baada ya watangazaji wao wazoefu kuacha kazi.

Uongozi wa Radio Free Africa uliendelea kutoa maelezo yake ya utetezi wa mdomo kama ifuatavyo:-

4.1 **Michael Noel** ambaye alitangaza kipindi hicho alianza kwa kukiri kosa kuwa ni kweli alisoma habari za magazetini kwa undani kinyume na agizo la Mh. Waziri. Aliendelea kujitetea kuwa alitenda kosa hilo kwa sababu ya kutokuwa na uzoefu na uelewa wa miongozo ya kimaudhui ya kipindi cha magazeti kwa kuwa siku hiyo alipangiwa kuendesha kipindi hicho kwa dharura baada ya watangazaji wazoefu wa kipindi hicho kuwa wameacha kazi kwa ghafla. Aliiomba radhi Kamati na kusema kuwa viongozi wake wameshamuelekeza, ameshajirekebisha na hatorudia tena kosa hilo.

4.2 **Steve Diallo,** Meneja Uendeshaji na Ufundi wa Radio Free Africa alianza kwa kuiomba radhi Kamati akidai kuwa chombo chenye uzoefu kama chao hakikupaswa kutenda kosa kama hilo. Alielezea kuwa kwa sasa kituo chao kinapitia wakati mgumu ambapo watangazaji wao wazoefu wamekuwa wakiacha kazi ghafla na hivyo wanawapa vijana wao wapya nafasi ya kukua zaidi. Alizidi kuomba radhi na kusisitiza kuwa mtangazaji wao tayari ameshajirekebisha na kuahidi kwamba kosa hilo halitajirudia tena katika kituo chao.

## 5.0 Majumuisho ya Utetezi

Katika kujumuisha utetezi wao, wote **Steve Diallo** na **Michael Noel** waliendelea kuiomba radhi Kamati kwa kosa lililofanyika na kuahidi kuwa watazidi kujirekebisha na kuboresha zaidi vipindi vyao kwa kuzingatia maadili.

## 6.0 Tathmini ya Kamati

6.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba, kituo cha Radio Free Africa kupitia kipindi chake cha Good Morning Africa kimekiuka agizo la Serikali la kutosoma habari za magazetini kwa undani kwa makusudi na pia utetezi wake haukuwa wa msingi;

6.2 Kamati ya Maudhui imeona kuwa utetezi wa kwamba mtangazaji wa Radio Free Africa aliendesha kipindi hicho kwa dharura bila kujua miongozo ya kimaudhui haukuwa wa msingi kwa kuwa msimamizi wa kipindi alitakiwa kuwa makini, na alitakiwa hata kuingia studio kumsimamisha mtangazaji asiendelee kufanya kosa kwa sababu kipindi kilichukua muda. Pia, Kamati imeona kuwa Radio Free Africa walipaswa kuwa wamesambaza Sheria, Kanuni, na miongozo yote ya Serikali kwa watangazaji wake wote ili kila mmoja aifahamu vizuri;

6.3 Hata hivyo, Kamati imeridhishwa na kitendo cha Radio Free Africa kutambua kosa lake, kulikiri, kujirekebisha na kuahidi kutolirudia tena.

## 7.0 Ushauri wa Kamati kwa Radio Free Africa

Kutokana na udhaifu uliobainika Kamati inaushauri uongozi wa Radio Free Africa kufanya mambo yafuatayo:

7.1 Kuimarisha na kuboresha usimamizi wa vipindi vyao;

7.2 Wafanye maandalizi na matayarisho ya kutosha ya vipindi vyao. ~~vya magazeti na hata kuruhusu mijadala ya wasikilizaji wao kwenye kipindi cha mjadala badala ya kusoma habari za magazeti kwa undani;~~

7.3 Kuwa na utaratibu wa kuwafanyia mafunzo ya awali (Induction Training) wafanyakazi wake wapya ili wapate uelewa wa Sheria, Kanuni, taratibu na miongozo yote ya Serikali wanapotekeleza majukumu yao katika tasnia ya habari;

7.4 Kuweka maagizo yote ya utendaji katika sehemu zilizo wazi ili watendaji wao waweze kuyaona, kuyasoma na kuyazingatia ipasavyo.

**8.0 Uamuzi wa Kamati**

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa Radio Free Africa, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa kituo cha Radio Free Africa kupitia kipindi chake cha Good Morning Africa, kipengele cha Tuzungumze Magazetini kimekiuka kwa makusudi agizo la Serikali la kutosoma habari za magazetini kwa undani kama ilivyoelezwa katika tathmini hapo juu.

Hivyo, Kamati ya Maudhui inaamua kukipa **Onyo** kituo cha Radio Free Africa na kukiagiza kutorudia kosa kama hili.

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam siku hii ya tarehe **15** mwezi **Aprili**, mwaka **2019**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Bi Valerie Ndeneingo-Sia Msoka**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

..............................................................

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Bwana Joseph Method Mapunda** ......................................
2. **Bwana Abdul Ramadhani Ngarawa**......................................
3. **Bwana Derek Kaitira Murusuri**......................................
4. **Bwana Jacob Gregory Tesha**......................................